K.J.S.E.A

# TATHMINI YA SHULE YA JUNIA
# TATHMINI YA MWISHO WA MUHULA WA 2, 2026
# GREDI YA 8 - KISWAHILI YA PILI
# Muda: Saa 1 Dakika 30

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

Jina: ______________________________ Shule: ______________________________

Nambari ya Tathmini: ______________________________ Tarehe: ______________________________

Nambari ya Shule: ______________________________ Sahihi: ______________________________

**MAELEKEZO KWA WANAFUNZI**

1. Andika jina lako, jina la shule yako na nambari yako ya mthani katika nafasi ulizoachiwa.
2. Andika tarehe,nambari ya shule yako kisa weka sahihi yako.
3. Soma kila swali kwa makini
4. Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote kwenye kijitabu hiki zimepigwa chapa.
5. Jibu maswali yote katika kijitabu hiki.

## JEDWALI LA ALAMA

| ZOEZI | INSHA | FASIHI | NOVELA | ASILIMIA (%) | KUZ 1 | KUZ 2 | KUF 1 | KUF 2 | KUK 1 | KUK 2 | CHI 1 | CHI12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KIWANGO CHA ALAMA | ALAMA 15 | ALAMA 15 | ALAMA 20 | | 90-10 0 | 75-89 | 58-74 | 41-57 | 31-40 | 21-30 | 11-20 | 1-10 |
| POINTI | | | | | 8 POINTI | 7 POINTI | 6 POINTI | 5 POINTI | 4 POINTI | 3 POINTI | 2 POINTI | 1 POINT I |
| JUMLA YA ALAMA ZA MWANAFUNZI | | | | | | | | | | | | |

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

## SEHEMU YA A: KUANDIKA (alama 15)

Andika barua kwa taasisi ya elimu ukiomba msaada wa vitabu vya ziada kwa shule yenu.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**SEHEMU B (Alama 35)**

**ZOEZI II: FASIHI SIMULIZI (alama 15)**

Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Zamani za kale, kobe alikuwa mnyama aliyetembea haraka sana. Aliweza kukimbia hata zaidi ya swara na paa. Alijivunia sana na kuwakejeli wanyama wengine waliotembea polepole.

Siku moja, kobe alifanya shindano la mbio na simba. Wanyama wote walikusanyika kushuhudia. Kabla ya mbio kuanza, kobe alimtukana simba na kusema, "Simba, wewe ni mfalme wa msitu lakini huna kasi. Nitakufundisha adabu leo!"

Simba hakupendezwa na maneno hayo, lakini alijizuia na kusema, "Twende, tutakutana uwanjani." Walipoanza kukimbia, kobe alikimbia sana hadi akaanguka kwa kishindo. Mguu wake ukavunjika na mgongo wake ukapasuka. Tangu siku hiyo, mgongo wake ukaonekana kuwa na mipasuko na akaacha kukimbia kabisa.

Wanyama walimcheka kobe, na tangu hapo akaamua kuwa mpole na kutembea taratibu ili asipate aibu tena.

(a) Hadithi hii ni mfano wa hurafa. Eleza sababu mbili zinazoonyesha hivyo. (Alama 2)

i. ____________________

ii. ____________________

(b) Eleza ujumbe mmoja unaopatikana katika hadithi hii. (Alama 2)

(c) Taja na ueleze kipengele kimoja cha uwasilishaji kilichotumika katika hadithi hii. (Alama 2)

(d) Tofautisha kati ya hadithi ya hurafa na ya hekaya (Alama 6)

| hadithi ya hurafa | hadithi ya hekaya |
|---|---|
| | |

(e) Taja sifa tatu za hadithi za hekaya (Alama 3)

i. ____________________

ii. ____________________

iii. ____________________

**ZOEZI III: NOVELA (ALAMA 10)**

**Soma sehemu ifuatayo ya novela kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Jioni hiyo, utulivu ulitanda katika kijiji cha Lulindi, upepo mwanana ukivuma taratibu huku watoto wakicheza pembeni mwa shamba la mahindi. Lakini mioyoni mwa wengi, kulikuwa na hofu na sintofahamu – hasa kwa vijana waliokuwa wakipotea kwenye ulevi, uvivu na tamaa.

Katika kijiji hicho aliishi Baraka, kijana mchanga mwenye ndoto tofauti. Alikuwa amerejea kutoka chuo kikuu akiwa na ari ya kubadili mtazamo wa rika lake. Aliona jinsi wazazi walivyolalamika kuhusu watoto wao, na jinsi wazee walivyolalamika kuwa heshima imetoweka.

Kwa msaada wa Mwalimu Janeth, aliyewahi kumfundisha akiwa mdogo, Baraka alianza kutoa mafunzo ya bure kila jioni chini ya mti mkubwa wa mkuyu. Alifundisha kuhusu nidhamu, ndoto, maarifa ya kilimo, na hata biashara ndogo ndogo. Vijana waliomsikia mwanzoni walimcheka, lakini wachache walianza kujitokeza.

Kadri wiki zilivyopita, kundi lake lilikua. Vijana waliokuwa wametelekeza mashamba yao walianza kulima, wengine wakaanzisha vikundi vya ufundi. Baraka hakuhubiri tu – alihamasisha kwa matendo.

Siku moja, wakati wa mkutano wa kijiji, wazee walimpongeza Baraka kwa kuwa mbegu ya mabadiliko. Alipewa jukumu rasmi la kuongoza baraza la vijana. Kijiji cha Lulindi kilianza kubadilika – kutoka kwenye giza la kukata tamaa hadi mwangaza wa matumaini.

(a) Andika anwani mwafaka kwa Novela hii. (Alama 1)

______________________________________________

(b) Taja mhusika mkuu katika Novela hii. (Alama 1)

______________________________________________

(c) Tambua na ueleze sifa nne za mhusika mkuu. (Alama 8)

i. ______________________________________________
ii. ______________________________________________
iii. ______________________________________________
iv. ______________________________________________

**TAMTHILIA (Alama 10)**

**Soma sehemu ifuatayo ya tamthilia kisha ujibu maswali yanayofuata.**

**Amani:** Bwana Juma, umeona hali ya nyumba yetu? Kila kona imeanza kuchafuka, na hiyo inaweza kuleta magonjwa kwa familia.

**Juma:** Ndio, Amani, lakini kazi nyingi na majukumu ya shambani yamenifanya nishindwe kuzingatia usafi kila siku. Mara nyingine huwa sina nguvu wala muda.

**Amani:** Naelewa, lakini usafi si lazima uwe mzito au mgumu. Tuwe na ratiba rahisi ya kusafisha kila siku, hata kidogo kidogo, ili tusije tukapata shida kubwa baadaye.

**Juma:** Labda unayo njia nzuri ya kutengeneza ratiba hiyo. Pia, nataka watoto waje watusaidie, siyo tu sisi wazazi.

**Amani:** Hiyo ni wazo zuri sana! Kujifunza usafi na pia kujifunza nidhamu. Watoto wakijihusisha, itakuwa rahisi kwetu sote, na pia wanajifunza kuwajibika.

**Juma:** Kweli, usafi wa nyumba si tu kwa afya, bali pia ni heshima kwa wageni na hata kwa wenye nyumba wenyewe.

**Amani:** Bila shaka. Usafi ni msingi wa maisha bora na amani ya familia. Tukifanya kazi kwa pamoja, tutakuwa na nyumba safi na furaha zaidi.

**Juma:** Nitajitahidi kuleta mabadiliko hayo, Amani. Hii ni changamoto tunayoweza kushinda iwapo tutazingatia umoja na ushirikiano.

(a) Taja wahusika wawili katika tamthilia hili na ueleze uhusiano wao wa kifamilia. (Alama 2)

i. ______________________

ii. ______________________

(b) Eleza jambo ambalo Amani anazungumzia kwa msisitizo katika mazungumzo haya. (Alama 2)

i. ______________________

ii. ______________________

(c) Jadili sifa mbili za Amani kama zinavyoonekana katika mazungumzo haya. (Alama 2)

i. ______________________

ii. ______________________

(d) Eleza wazo moja kuu unalojifunza kutokana na tamthilia hili. (Alama 2)

______________________

______________________

(e) Kwa maoni yako, kwa nini Juma anasema: "Nitajitahidi kuleta mabadiliko hayo, Amani"? (Alama 2)

i. ______________________

ii. ______________________

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**

**MAJIBU**

**BARUA YA KIKAZI**

Shule ya _____________
S.L.P _____________
Mji _____________
Tarehe _____________

Mkurugenzi wa Elimu,
Wizara ya Elimu,
S.L.P _____________
Nairobi.

**YAH: MAOMBI YA MSAADA WA VITABU VYA ZIADA KWA SHULE YETU**

Natumai barua hii itakufikia ukiwa na afya njema. Nimeandika barua hii kukuomba msaada wa vitabu vya ziada kwa ajili ya shule yetu.

Shule yetu ina idadi kubwa ya wanafunzi, na vitabu vilivyopo havitoshelezi mahitaji ya wanafunzi wote. Hali hii imekuwa changamoto kwa wanafunzi kwani wengi hulazimika kushiriki kitabu kimoja, jambo linalopunguza ufanisi katika masomo.

Tunaomba taasisi yako itusaidie kwa kutupatia vitabu vya ziada katika masomo mbalimbali kama Kiswahili, Kiingereza, Hisabati na Sayansi. Vitabu hivi vitasaidia kuboresha matokeo ya wanafunzi na kuinua kiwango cha elimu katika shule yetu.

Tutashukuru sana endapo ombi letu litazingatiwa kwa haraka. Tunatarajia msaada wenu muhimu kwa maendeleo ya elimu ya wanafunzi wetu.

Wako mwaminifu,



(Mwanafunzi / Mkuu wa Darasa)

**ZOEZI 2: FASIHI SIMULIZI**

(a)

- Inahusisha wanyama wanaozungumza kama binadamu.
- Inafundisha maadili kupitia visa vya kubuni.

(b)

- Kiburi na kujivuna huleta aibu na hasara.

(c)

- Mazungumzo: Simba na kobe wanazungumza kama binadamu.

(d)

- Hadithi ya hurafa hutumia wanyama kuonyesha maadili kwa visa vya kubuni.
- Hekaya ni hadithi za kuburudisha na zinaweza kumhusu binadamu au mnyama bila kuzingatia maadili.
- Hurafa hutoa funzo au onyo, hekaya huzingatia burudani na maajabu.

(e)

- Husimulia visa vya kubuni.
- Hutumia lugha ya kuvutia na ya picha.
- Huwa na mafundisho au maadili.

## ZOEZI 3: NOVELA

(a) **Mbegu ya Mabadiliko**
(b) **Baraka**
(c)

- Mwadilifu: Alijali jamii yake.
- Mhamasishaji: Aliwahimiza vijana kubadilika.
- Mwenye nidhamu: Alifundisha nidhamu na maarifa.
- Jasiri: Alikabiliana na upinzani na mzaha wa vijana.

## TAMTHILIA

(a) Amani na Juma – ni mume na mke.
(b) Umuhimu wa kudumisha usafi wa nyumba ili kuepuka magonjwa.
(c)

- Mwenye busara: Anashauri kwa utulivu na kueleza kwa upole.
- Mshauri: Anapendekeza suluhisho la pamoja na kushirikisha familia.

(d) Usafi ni wajibu wa familia yote na msingi wa afya na heshima.
(e) Kwa sababu ametambua umuhimu wa usafi na anataka kubadilika kwa manufaa ya familia yake.